OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

SHULE YA SEKONDARI MBAGALA KUU
S. L. P. 46357, TEMEKE – DAR ES SALAAM

Jina la mwanafunzi **…….....** Na ya fomu **……..**

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBAGALA KUU WILAYA YA TEMEKE, MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA ……

1.0. Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **Kwanza** katika shule hii mwaka **2021** Shule ya Sekondari Mbagala ipo umbali wa kilometa nane (08) mashariki mwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Usafiri wa basi kutoka Mbagala Rangi tatu unapatikana katika kituo cha mabasi cha Zakhem. Nauli ni Tshs mia nne/mia mbili (400/200).

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021**

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **04/1/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/01/2021** Ndani ya siku saba.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare za Shule

NA.	WAVULANA	WASICHANA
1.	Suruali za kijani, rinda mbili pande zote, mifuko miwili pembeni na mmoja nyuma.(sample ya kipande cha kitambaa kitapatikana shule)	Sketi 2 za kijani mshono rinda box urefu wa kutosha kuanzia nchi 6 kutoka kwenye goti. .(sample ya kipande cha kitambaa kitapatikana shule)
2.	Mashati 2 meupe yasiyo bana au mafupi au makubwa sana.	Mashati 2 meupe yasiyo bana au mafupi au makubwa sana.
3.	Soksi nyeusi jozi mbili (2)	Soksi nyeupe jozi mbili (2)
4.	Mkanda mweusi wa ngozi usio na marembo wenye baco ndogo wa kawaida	Nusu kanzu na Hijabu nyeupe, inatakiwa kuziba sehemu ya tumbo na sio kifua tu.
5.	Viatu vyeusi vya ngozi visivyochongoka mbele visivyo na marembo (sio mocasine) viwe na kisigino kifupi	Viatu vyeusi vya ngozi visivyochongoka mbele visivyo na marembo viwe na kisigino kifupi
6.	Bukta ya michezo na T-Shirt ya kijani	Bukta ya michezo na T-Shirt ya kijani
7.	Raba za michezo nyeupe	Raba za michezo nyeupe
8.	Sweta la kijani lenye umbo la V shingoni	Sweta la kijani lenye umbo V shingoni.

2.2. Mahitaji mengine

NA.	WAVULANA	WASICHANA
1.	Mathematical set 1 (kopo la vifaa vya hesabu)	Mathematical set 1 (kopo la vifaa vya hesabu).
2.	Daftari kubwa 11 (Counter book three quire)	Daftari kubwa 11 (Counter book three quire)
3.	Kalamu za kutosha, rula, penseli na vifutio	Kalamu za kutosha, rula, penseli na vifutio
4.	Begi la kubebea madaftari la mgongoni	Begi la kubebea madaftari la mgongoni

2.3. Umpe mwanao nauli ya kwenda na kurudi kila siku na fedha ya kununua chakula ikibidi.

3.0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii
Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 mwaka ya 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(i) Kutunza mali za umma

3.1. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule
(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kudharau Bendera ya Taifa
(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kuwa na simu ya mkononi

KILA WAKATI FIKIRI KWANZA KABLA YA KUNENA
NA TUMIA BUSARA KABLA YA KUTENDA

4.0. Adhabu

i) Adhabu zinaweza kutolewa na mwalimu yeyote kwa mwanafunzi anayeonyesha utovu wa nidhamu

ii) Kiranja pia anaruhusiwa kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendeka na mwanafunzi ili mradi asipige kiboko au kuzuia kuingia darasani wakati wa masomo

iii) Kosa linapokuwa kubwa litaandikwa katika jalada la mwanafunzi na kitabu cha kumbukumbu za adhabu (black book) hata hivyo mkuu wa shule ataidhinisha adhabu
zinazotolewa kwa wanafunzi.

5.0 Mambo mengine muhimu

a) "Medical Examination Form" ambayo itajazwa na mganga Mkuu hospitali ya Serikali ya Wilaya. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule utakaporipoti shuleni

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada /michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule nayo itakabidhiwa.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

TIMIZA WAJIBU WAKO FUATA KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

.....
MKUU WA SHULE

KARIBU SANA MBAGALA KUU SEKONDARI

Kiambatanisho A

Makubaliano

Simu……

Tarehe: …….

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MBAGALA KUU
S. L. P. 46357,
DAR ES SALAAM.

YAH: KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE

Mimi ……. wa kidato cha ……. Mwaka ……
Naikubali nafasi hii na nitatii sheria za shule zilizopo na zile zote zitakazotolewa kwa muda wowote. Aidha naahidi kuwatii walimu, wafanyakazi wasio walimu na viongozi watakaochaguliwa kwa mujibu wa sheria. Ninakiri kuwa sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Nitatunza mali ya Umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu na vifaa vya maabara.Pia nitatoa ushirikiano kuwafichua wanafunzi wanaoharibu mali ya umma.

Ninaahidi kuwa mwaminifu na kwamba, nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu wote kwa manufaa yangu na Taifa letu kwa Ujumla
"MUNGU NISAIDIE"
Sahihi …….. **Tarehe ……**

AHADI YA MZAZI/MLEZI
Mimi Mzazi/Mlezi wa ……ninaahidi kwamba:-
1. Nitampatia mwanangu mahitaji yote ya shule kama yalivyotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule.
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu.
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (Home work) na kufuatilia maendeleo yake shuleni. Mwanangu ataingia kusoma vipindi vya dini ya ……. Dhehebu la …….
4. Mwanafunzi akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake. Nitasimamia mahudhurio yake ipasavyo na nitahakikisha kuwa amefika shuleni kabla ya saa 1:00 asubuhi kila siku ya masomo.
5. Kutoa taarifa iwapo mwanafunzi anabadilishiwa makazi/mlezi kwa uongonzi wa shule.
6. Nitaitikia wito wa walimu mara tu nitakapoitwa na nitahudhuria vikao kwa ajili ya maendeleo ya mwanangu.
7. Endapo sitatimiza wajibu wangu kwa hayo niliyoelekezwa 1,2,3,4,5,6, hatua nyingine za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Jina la Mzazi/Mlezi…… **Sahihi……**

UTHIBITISHO:-
M/Kiti wa Mtaa. Nathibitisha kwamba ndugu……
ni mkazi wa eneo la …….. Jina: ……

Sahihi: …….. **Cheo: ……**

Kiambatanisho B

SHULE YA SEKONDARI YA MBAGALA KUU
FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI

PICHA

A. IJAZWE NA MWANAFUNZI

1. Majina kamili: …….
2. Tarehe ya Kuzaliwa: …….
3. Mvulana/Msichana: ……
4. Uraia: ……
5. Dini: ……...
6. Shule aliyotoka kabla ya kuja shule ya Sekondari Mbagala kuu

Shule ya Msingi/Sekondari	Tarehe na mwaka ulioanza	Tarehe na mwaka uliotoka
Msingi……..		
Sekondari……..		

Sahihi ya mwanafunzi…….. Tarehe: ……

B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……..
2. Uraia: …….
3. Anuani ya DSM ……
4. Sehemu anayoishi: …….
5. Mtaa: …….
6. Namba ya nyumba: ……
7. Simu Ya nyumbani /Mkononi 1……
   2 ……

PICHA

Eleza kama mtoto ana matatizo mengine tofauti na yaliyopo katika kiambatanisho C (fomu ya hosptali)

……..
……...

C. MAELEZO YA KIKAZI

i) Jina la mwajiri: ……
ii) Anwani: ……
iii) Kazi ya Mzazi/Mlezi: …….
(mfano, Karani, Mwalimu n.k)

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: …… Tarehe: ……..

Kiambatanisho C

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MBAGALA KUU SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be filled by Government Medical Officer and return to the Head of School Mbagala kuu Secondary School P.O. Box 46357,DSM.
This form have to be filled correctly

To the Medical Officer,

……

……

……

RE: Mr/Miss ……..

Please examine the above mentioned student. Comment on his/her fitness by responding to the problems below put a tick (√) for positive and a cross (x) for negative ……against in a box provided.

HEAD MASTER/HEAD MISTRESS **Date: …….**

Insert (√) in the boxes provided

1. Hearing	YES	☐	NO	☐
2. Pregnancy	YES	☐	NO	☐
3. Speech	YES	☐	NO	☐
4. Asthma	YES	☐	NO	☐
5. Sight	YES	☐	NO	☐
6. T.B(Tuberculosis)	YES	☐	NO	☐
7. Sickle cell	YES	☐	NO	☐
8. Mental case	YES	☐	NO	☐
9. Physical Disability	YES	☐	NO	☐

10. Any other problem……

MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by a medical officer)
I have examined the above named student and consider that he/she is physically FIT/UNFIT for admission as above

……

Name: …… Signature: ……

Designation & Stamp Date: ……